**JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)

**12 AGOSTI, 2022**
**DODOMA**

***Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Waziri wa Madini;***

***Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri Mliopo;***

***Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;***

***Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;***

***Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge Mliopo;***

***Waheshimiwa Wabunge Mliopo;***

***Makatibu Wakuu wote mliopo wakiongozwa na Bw. Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu Wizara ya Madini;***

***Mej. Jen. Mst. Michael Isamuhyo, Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO;***

***Dkt. Venance Mwasse, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO;***

***Prof. Idris Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini;***

***Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali mliopo;***

***Viongozi wa Dini Mliopo;***

***Watumishi wa STAMICO;***

***Wadau wa Sekta ya Madini;***

***Ndugu Wanahabari;***

***Mabibi na Mabwana;***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha katika tukio hili muhimu la kuadhimisha Miaka 50 ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). Nawapongeza Menejimenti ya Wizara pamoja na STAMICO na watumishi wote kwa kufikia hatua hii. Pia, hongereni kwa kufanikisha Maadhimisho haya na ushiriki wenu katika shughuli za kijamii ikiwamo ya upandaji wa miti.

Aidha, napenda kuwapongeza STAMICO kwa kazi nzuri mnayoifanya, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1972. Imeelezwa hapa kuwa hivi karibuni Shirika limeweza kufanya mapinduzi makubwa ya kiutendaji, kuongeza ubunifu,

kuimarisha uzalishaji na kujenga misingi mizuri ya kujiendesha kibiashara na kupunguza utegemezi wa moja kwa moja kwa Serikali. **Hongereni sana!**

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kujipambanua kuhusu dhamira yake ya kuhakikisha Sekta ya Madini inakua kwa kasi kubwa, inatoa ajira kwa Watanzania wengi zaidi na kuchangia zaidi katika Pato la Taifa.

Mwaka 2019, kabla ya janga la UVIKO-19, Sekta ya Madini ilivunja rekodi kwa kukua kwa asilimia 17.7 ukilinganisha na sekta nyingine. Aidha, pamoja na athari za janga hilo, Sekta ya Madini imeendelea kuwa imara ambapo mwaka 2021 ilikua kwa asilimia 9.6. Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 7.2 mwaka 2021 kutoka asilimia 6.7 mwaka 2020 na asilimia 4.3 mwaka 2015. Fedha za kigeni kutoka katika Sekta ya Madini zimefikia dola za Marekani bilioni 3.1 kwa mwaka 2021/22, sawa na takribani asilimia 43 ya fedha zote za kigeni zitokanazo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi katika kipindi hicho. Lengo la Serikali kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ni kuona mchango wa sekta hiyo unafikia asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025/26 na kuingiza fedha za kigeni takriban dola za Marekani bilioni 5.5 kwa mwaka. Tunaamini tukiendelea na juhudi hizi tunaweza kufikia malengo hayo.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Kaulimbiu ya Maadhimisho haya ya Miaka 50 ya STAMICO inasema **"*STAMICO kwa Ukuzaji wa Sekta ya Madini.*"** Kaulimbiu hii inatukumbusha kuwa, ukuaji wa sekta ya madini unategemea, pamoja na mambo mengine, mwenendo wa utendaji wa STAMICO. Hivyo, kama Shirika mmepewa dhamana kubwa ya kusimamia sekta ya madini kwa niaba ya watanzania, na kuhakikisha tunafikia malengo yaliyokusudiwa. Hamna budi kuendelea kusimamia dhamana hiyo kwa weledi na uadilifu kwa manufaa ya Taifa letu. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alianzisha Shirika hili kwa lengo la kuwajengea Watanzania ujuzi na uwezo wa kumiliki na kusimamia Sekta ya Madini kwa maslahi ya Taifa. Ili tuweze kunufaika na madini tuliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu, hatuna budi kushiriki kikamilifu katika mnyororo wa thamani wa madini toka katika hatua ya utafutaji, uchorongaji, uchimbaji, uchenjuaji, uongezaji thamani na biashara ya madini.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza STAMICO kwa jitihada mlizofanya kutekeleza majukumu yenu na kuweza kupata mafanikio ya kuridhisha. Kwa mfano, kupitia vituo vyenu vitatu vya mfano kwa wachimbaji wadogo, vya Lwamgasa, Katente na Itumbi, mmeweza kutoa mafunzo kwa vitendo kuhusu utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini, utunzaji wa mazingira na takwimu za kifedha. Uwekezaji huu umeongeza uwezo na umewasaidia wachimbaji wadogo kuanza kukopesheka. Pia, nimeelezwa kwamba Shirika limeendelea kuwekeza na kuboresha miradi yake ya kuzalisha makaa ya mawe kule Kiwira kwa kuanza uchimbaji na uuzaji wa makaa kwa wastani wa tani elfu sitini kwa mwezi ndani na nje ya nchi. Vilevile, mmenunua mitambo 11 ya uchorongaji ambayo imeliwezesha Shirika kuingia katika mikataba ya uchorongaji katika migodi ya Geita Gold Mine (GGM), Buckreef Gold Mine, Buhemba Gold Mine na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania - *Tanzania Geothermal Development Company (TGDC)*. Hali kadhalika, mmeimarisha uzalishaji katika mgodi wa dhahabu wa STAMIGOLD pamoja na kuimarisha kampuni za ubia.

Aidha, nawapongeza kwa kujiongeza, kubuni na kuanzisha miradi mipya ya kutengeneza nishati mbadala kutokana na makaa ya mawe kwa ajili ya kupikia mliyoipa jina la *Rafiki Briquettes* ambao nitaufungua rasmi leo. Kwa hakika, aina hii ya nishati italeta mapinduzi makubwa katika sekta ya nishati nchini kwa kupunguza matumizi ya mkaa wa miti na kuni, hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira. Natoa wito kwa Watanzania wote, ikiwamo taasisi za Serikali kuchangamkia mkaa huu ambao ni rafiki kwa mazingira. Nawasihi STAMICO muendelee kuongeza ufanisi katika usimamizi na uzalishaji katika miradi yenu yote na kuanzisha miradi mipya ya kimkakati hususan ya kuongeza thamani kupitia leseni zenu. *Fursa zipo nyingi sana!* Kama STAMICO na wawekezaji wote walio na leseni za madini nchini mtajielekeza kuongeza thamani ya madini, hakika Tanzania itapiga hatua kubwa sana. Kwa upande wa Serikali tutaendelea kutatua changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji, miundombinu ikiwamo upatikanaji wa maji na nishati ya kutosha, huduma za mawasiliano na usafirishaji. Aidha, Serikali itaendelea kuiwezesha STAMICO kuongeza ujuzi wa nguvukazi iliyopo na kuajiri wataalam na watumishi wanaohitajika katika uzalishaji ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Kutokana na uwekezaji na fikra za kijasiriamali, STAMICO imeongeza kasi kuelekea kujiendesha kibiashara hususan katika miaka ya hivi karibuni ambapo mapato ya jumla yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1.36 mwaka 2018/19 hadi

shilingi bilioni 48.45 mwaka 2021/22. Kutokana na mapato hayo utegemezi wa Shirika kwa Serikali umepungua kutoka asilimia 89 mwaka 2018/19 hadi asilimia 13.2 mwaka 2021/22 na kuliwezesha Shirika kutoa gawio la shilingi bilioni 1.2 kutokana na faida kwa mara ya kwanza. Aidha, mwaka 2020/21 Shirika limetengeza faida ya shilingi bilioni 4.3 na hapa nimenong'onezwa kwamba mwaka 2021/22 Shirika linatarajia kukusanya mapato ya ndani kiasi cha shilingi billion 70. Haya ni mafanikio mazuri na ya kutia moyo. **Hongereni sana!**

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Pamoja na mafanikio ya STAMICO na Sekta ya Madini kwa ujumla katika kipindi cha nusu karne, yako maeneo kadhaa ambayo hayana budi kuboreshwa. Hivyo basi, kupitia hadhara hii napenda kuelekeza mambo yafuatayo:

***Jambo la Kwanza***, bado shughuli za uchimbaji madini hazizingatii ipasavyo suala la uhifadhi wa mazingira. Matumizi ya zebaki na kemikali mbalimbali yameendelea kuchafua mito, maziwa na mazingira kwa ujumla na kuhatarisha maisha ya watu, uzalishaji wa mazao, mifugo na hata upatikanaji wa samaki. Wizara ya Madini, STAMICO na NEMC ninawaagiza muongeze kasi ya ukaguzi wa migodi mikubwa na midogo ili kuwabaini na kuwachukulia hatua za kisheria wachimbaji madini wanaozembea na kuharibu au kuchafua mazingira. Aidha, ni muhimu pia elimu ya kutosha itolewe juu ya madhara makubwa ya uchafuzi wa mazingira kwa maisha ya binadamu na viumbe vingine hai na uendelevu wa ikolojia.

**Jambo la Pili**, Kumekuwa na changamoto ya kuongezeka kwa wagonjwa kutoka katika migodi ya madini ambao wanaathirika na vumbi linalotokana na shughuli za uchimbaji madini. Katika Hospitali yetu ya Kibong'oto iliyopo Wilaya ya Siha, kwa siku kuna wastani wa wagonjwa 25 waliolazwa, wengi wao wakiwa vijana kati ya miaka 20 hadi 40, ambao wameathirika na vumbi linalotokana na shughuli za uchimbaji wa madini.  Wagonjwa hawa wanatumia takribani mitungi 30 ya hewa tiba ya oksijen kwa siku na hivyo kugharimu Serikali zaidi ya shilingi million 500 kwa mwaka kwa hospitali hii moja tu. Baadhi yao wapo hospitalini pale kwa zaidi ya miaka miwili wakipumulia mashine. Nilielezwa kuwa, vumbi la migodini lina **'silica' (ulanga)** ambayo ikiingia katika mfumo wa upumuaji husababisha ugonjwa wa ***Silicosis***. Ugonjwa huu unaathiri mapafu na madhara yake ni pamoja na kupata saratani ya mapafu, kufeli kwa figo na moyo, na pia ni kichocheo kikubwa cha maambukizi ya ugonjwa wa Kifua kikuu ambao ni tishio kwa Taifa letu. Utafiti uliofanywa na Hospitali hiyo ya Kibong'oto pamoja na Chuo Kikuu cha KCMC kwenye **migodi 22 ya Mererani Wilayani Simanjiro** ulionesha kiwango cha silica kwenye vumbi linalovutwa na wachimbaji kilikuwa ni

wastani wa miligramu **1.227** kiwango ambacho ni kikubwa zaidi ya mara 25 ya kiwango kinachokubalika kimataifa cha miligramu **0.05.** Aidha, utafiti uliofanywa kwa wachimbaji **330** katika migodi ya Mererani mwaka 2021, matokeo ya awali yanaonesha wachimbaji **99** sawa na asilimia **30** walikuwa wameathirika na ugonjwa wa *Silicosis* na wachimbaji **20** sawa na asilimia **6.1** walikuwa na ugonjwa wa **Kifua kikuu** hii ikiwa ni **mara 24** zaidi ya wastani wa kitaifa.

Hivyo, nawataka Wizara ya Madini mshirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; na Wizara ya Afya kuhakikisha sheria na kanuni za afya na usalama mahala pa kazi zinafuatwa na pia muweke haraka utaratibu utakaowezesha kudhibiti changamoto hiyo. Aidha, toeni elimu kwa wamiliki wa migodi na wachimbaji kuhusu namna bora ya kujikinga na vumbi wanapokuwa katika shughuli za uchimbaji wa madini ikiwemo uvaaji wa barakoa wakati wa kazi, unyunyiziaji wa maji ili kupunguza vumbi na kuhakikisha mzunguko wa hewa unapatikana katika maeneo ya kazi. Kadhalika, nawataka Tume ya Madini kusaidia fedha na vitendea kazi ili kuboresha afya za wachimba madini. Vilevile, Wizara ya Madini na Wakuu wa Mikoa yote yenye migodi ya madini nchini, viongozi wa chama cha wachimbaji pamoja na wamiliki wa migodi nawashauri mkatembelee Hospitali ya Kibong'oto kujionea hali ilivyo. Naamini mkijionea vijana wetu wanavyoteseka mtaguswa na kuchukua hatua madhubuti.

***Jambo la Tatu***, napenda kutoa rai kwa taasisi za fedha kuendeleza jitihada za kuweka masharti nafuu ya upatikanaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo wadogo na wa kati ili kuwasaidia kupata mitaji na zana za kisasa zitakazo wawezesha kuongeza tija, ajira na kufanya shughuli za uchimbaji kwa kutumia teknolojia rafiki na mazingira yanayowazunguka.

***Jambo la Nne***, STAMICO kwa kushirikiana na SIDO ongezeni jitihada za ubunifu ikiwa pamoja na kutengeneza zana bora za uchimbaji madini za gharama nafuu kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo ili kuongeza uwezo wao wa uzalishaji kwa tija zaidi na usalama wa wachimbaji wakiwa migodini.

***Jambo la Tano***, natoa wito kwa Mashirika mengine ya umma kuiga mfano wa STAMICO ambapo huko nyuma Shirika lilikuwa linasuasua kiutendaji lakini sasa limeanza kujikwamua. Napenda niwatahadharishe mapema kuwa Serikali inaendelea kufanya tathmini ya Mashirika yanayojiendesha kwa hasara na itachukua hatua stahiki kulingana na taarifa ya tathmini inayofanyika. Hivyo nawashauri, *mjipange kabla hamjapangwa!*

***Jambo la Sita***, Wizara ya Madini kwa kushirikiana na STAMICO na Halmashauri, hakikisheni ajira za watoto migodini wanaojulikana kama '*nyoka*' zinakomeshwa mara moja ili kulinda afya zao na kuwawezesha watoto hao kuendelea na masomo.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kuwaalika wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye Sekta ya Madini kwani fursa za kibiashara zipo za kutosha na Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara kwa amani na usalama. Tanzania bado ina hazina kubwa ya rasilimali madini ambayo haijaguswa na inahitaji uwekezaji. Hadi sasa tumeyafikia madini yetu kwa asilimia 10 tu ikilinganishwa na utajiri uliopo ardhini hapa nchini kwetu.

Mwisho kabisa naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kuwakumbusha kuwa tarehe 23 Agosti mwaka huu nchi yetu itaendesha zoezi la sensa ya Watu na Makazi. Hivyo, nawaomba wananchi wote tujitokeze kuhesabiwa. Nawasihi tusifiche idadi sahihi ya watoto, watu wenye ulemavu, wazee, wanawake, wanaume na kaya wanapoishi. Wote wanahitaji kuhesabiwa.

Baada ya kusema hayo sasa nipo tayari kuzindua nishati mbadala ya mkaa wa *Rafiki Briquettes*.

**STAMICO Oyee! Madini Oyee!**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**